A. HISTORIA YA PAROKIA YA MT.THOMAS MTUME

Parokia ya Mtakatifu Thomas Mtume ilianza mwaka 1982 kutoka katika Parokia ya Pugu, chini ya uongozi wa Padri Menhard, Mkapuchini. Wakati huo ilikuwa ikijulikana kama Kigango cha Mtakatifu Stephano Shahidi. Waamini walipewa ruhusa ya kutumia darasa la Shule ya Msingi Chanika kama mahali pa kusali pamoja. Waamini wengi walikuwa wa kabila la Wamakonde waliotokea eneo lililojulikana kama Msumbiji, ambalo kwa sasa linaitwa Chanika Mwisho. Kipindi hicho, kigango kilikuwa na takribani kaya 15 hadi 20 za waamini. Mwaka 1983, Padri Menhard, kwa kushirikiana na waamini, alitafuta eneo la kujenga kanisa kupitia uongozi wa kijiji. Walipatiwa kiwanja chenye ukubwa wa nusu ekari katika eneo la Nguvu Kazi, Chanika, mkabala na kituo cha afya cha Nguvu Kazi kilichokuwa kikitoa huduma za mama na mtoto.

Uamuzi wa kutafuta eneo hilo ulitokana na waamini kuzuiwa kuendelea kutumia darasa la shule kama mahali pa ibada. Mwalimu Mkuu wa shule aliwataka watafute sehemu nyingine ya kusalia. Hivyo, waamini walianza kujenga kanisa dogo katika eneo walilopewa, wakitumia nguvu zao pamoja na msaada wa watu mbalimbali. Ujenzi wa kanisa hilo dogo katika eneo la Nguvu Kazi kwa kushirikiana na waumini, pia na familia ya Padri Menhard (Kaka na dada yake walifika Chanika, wakasali pamoja na waamini na kutoa fedha kwa ajili ya ujenzi wa kanisa) walijitolea kwa ajili kukamilisha ujenzi.

Makatekista wa kwanza kuhudumu katika kigango hicho walikuwa Mzee Antony Ambasi na Antony Kobelo. Hivyo, historia ya Parokia hii inaanzia katika mchakato wa kuanzishwa kwa Kigango cha Mtakatifu Stephano Shahidi.

Kuhamishwa kwa Kigango kwenda Chanika Mwisho

Kigango kiliendelea kukua chini ya usimamizi wa Parokia ya Pugu. Mwaka 1992, Paroko mpya wa Pugu, Padri Stefano Oswald Nyilawila, alipendekeza Kigango kuhamishwa kutoka Nguvu Kazi kwenda Msumbiji, yaani Chanika Mwisho, ambako Kanisa la Parokia lilipo hadi sasa. Sababu kubwa ya kuhamishwa kwa Kigango ilikuwa kwamba waamini wengi, hasa wa kabila la Wamakonde, waliishi katika eneo hilo. Hatua hiyo ililenga kuwarahisishia waamini kupata huduma za kiroho. Muumini mmoja aliyeitwa Mzee Antony Ambasi alitoa eneo kwa ajili ya ujenzi wa kanisa. Mwanzoni, waamini walisali chini ya mti. Baadaye, walijenga kanisa la muda kwa kutumia miti na makuti.

Usimamizi wa Shirika la MCBS

Baada ya ujenzi wa kanisa dogo kukamilika, Shirika la Wamisionari wa Ekaristi Takatifu (**Missionary Congregation of the Blessed Sacrament – MCBS** kutoka India lilikabidhiwa usimamizi wa Kigango mnamo mwaka 2012, na Padri Leornardo Amadori-OFMCap akiwa Paroko wa Parokia ya Mt. Fransisco wa Azizi -Pugu, kwa niaba ya Baba Askofu Mkuu Jimbo Kuu la Dar es Salaam .

Baada ya kukabidhiwa jukumu hilo, Shirika lilipendekeza jina la Kigango libadilishwe kutoka Mtakatifu Stephano Shahidi – Chanika na kuitwa Mtakatifu Thomas Mtume – Chanika. Jina hilo lilichaguliwa kwa sababu Mtakatifu Thomas Mtume ndiye Mtume

aliyehubiri na kufia nchini India, na pia ni msimamizi wa nchi hiyo.

Kuanzishwa kwa Parokia

Tarehe 6 Januari 2013, Kigango kilitangazwa rasmi kuwa Parokia. Paroko wa kwanza alikuwa Padri Lijeesh Varghese, anayejulikana pia kama Padri Sebastian. Alisaidiwa na Paroko Msaidizi, Padri Jobin Chako, anayejulikana pia kama Padri Jacobo. Wakati huo, idadi ya familia za waamini ilikuwa imeongezeka hadi kufikia takribani 350. Parokia mpya ilikabidhiwa jumla ya vigango 10. Vigango sita vilitoka Parokia ya Kisarawe, ambavyo ni: Kiwambe,Homboza, Msimbu, Kitanga, Maji Chumvi, Mwanzo Mgumu. Vigango vinne vilitoka Parokia ya Pugu, ambavyo ni Yongwe, Zingiziwa, Mvuti na Msongola B.Vigango hivyo viliendelea kukua kiroho na kiuchumi. Baadhi yake baadaye vilitangazwa kuwa Parokia Teule na hatimaye kuwa Parokia Kamili.

Ujenzi wa Kanisa jipya

Mwanzo wa mwaka 2018, maandalizi ya ujenzi wa Kanisa yalianza na siku ya 16.09.2018 tulianza ujenzi rasmi wa Kanisa letu jipya ambalo limepitia katika hatua kuu tatu hadi leo unapolitabaruku: -

Na	Awamu	Kuanza	Kukamilika	Kazi zilizofanyika
1	Awamu ya kwanza	2018	2020	Kupima hali ya udongo kwa ajili ya kuanza Kujenga msingi, kuchimba na kujenga msingi, kuweka sakafu ya Kanisa na nguzo za Kanisa, Kujenga kuta za kanisa, Kujenga minara.
2	Awamu ya pili	2021	2023	Kupaua , Kuweka plasta na skimini
3	Awamu ya tatu	2023	2026	Kuweka Grili za madirisha, Vioo vya madirisha, kuweka domu juu ya altare, tarazo, milango, kuweka dari, pavumenti, ununuzi wa mabenchi, mifumo ya umeme,sauti na rangi.
4	Kutabaruku Kanisa na Altare	**31/10/ 2026**	Kutabaruku Kanisa na Altare	